

TAARIFA KWA UMMA

Ndugu waandishi wa habari,

Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kama zilivyo Halmashauri nyingine imeanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 [Marejeo ya Mwaka 2019], Sheria Namba 7 ya Mwaka 1982.

Ndugu waandishi wa habari,

Naomba kutoa majibu ya malalamiko ya wananchi kupitia **Gazeti la Mwananchi** la tarehe **22/05/2023** lililokuwa na malalamiko yafuatayo:- Halmashauri kutoza shs. **20,000/=** kwa ajili ya kulipia kibali cha mazishi na shs **20,000/=** kwa ajili ya kulipia kibali cha Harusi (Kugemula),

Ndugu waandishi wa habari,

Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kupitia Baraza la Madiwani lilitunga Sheria Ndogo za Halmashauri ili kurahisisha utendaji na ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.

Sheria Ndogo za Halmashauri zinaainisha vyanzo vya mapato na kiasi cha kulipia. Mapato yote ya Halmashauri hutozwa kupitia mashine za ukusanyaji (POS).

Ukiangalia mashine zetu za kukusanya mapato zina vyanzo vyote vya mapato kama vilivyo katika sheria ndogo na viwango vya ushuru au tozo ni sawa kabisa na vile vilivyoko kwenye Sheria Ndogo.

Katika orodha ya vyanzo vya mapato tulivyonavyo hatuna ushuru au ada ya shs. 20,000/= kwa ajili ya kulipia kibali cha mazishi na shs. 20,000/= kwa ajili ya kulipia kibali cha Harusi (Kugemula).

Ndugu waandishi wa Habari

Naomba kuisitiza tena kwamba Katika orodha ya vyanzo vya mapato tulivyonavyo hatuna ushuru au ada ya shs. 20,000/= kwa ajili ya kulipia kibali cha mazishi na shs. 20,000/= kwa ajili ya kulipia kibali cha Harusi (Kugemula).

Ikiwa kuna mtu atakutana na jambo kama hilo, naomba tupate taarifa mapema iwezekanavyo ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

MWISHO

Ndugu waandishi wa habari,

Napenda kuwashukuru wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya Buhigwe kwa ushirikiano ninaoupata ili kuhakikisha kwamba naendelea kutimiza majukumu yangu ya kuwahudumia.

Pia napenda kutumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wakuu wangu wa Divisheni na Vitengo pamoja na Watumishi wote wa Halmashauri ya Buhigwe kwa ushirikiano ninaoupata na uchapa kazi wenu ili kuhakikisha tunaendelea kuwatumikia wananchi wa Buhigwe.

Naomba niendelee kuwasihii wananchi kutueleza changamoto mbalimbali pindi zinapojitokeza ili watumishi wa umma tuendeleo kuwatumikia na kuwapatia huduma iliyo bora.

*Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki
Wilaya ya Buhigwe.*

“ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA”

Imetolewa na

Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano Serikalini
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE